JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 19- 2019/2020**

**DHIDI YA**

# WASAFI FM

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ilitoa leseni ya kurusha Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa kituo cha **WASAFI FM** kwa ajili ya kutoa huduma za uandaaji na utangazaji wa maudhui kwa njia ya redio.

1.2 Tarehe 22/04/2020, saa 2.00 asubuhi, kituo cha **WASAFI FM** kinatuhumiwa kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya utangazaji kupitia kipindi cha ***"Goodmorning Habari ya Asubuhi"***. Kipindi hicho kilikuwa na maudhui yenye lugha ya dhihaka, kashfa na kejeli.

1.3 Watangazaji wa kipindi cha ***"Goodmorning Habari ya Asubuhi"*** katika kipengele cha ***"Kurasa za Magazeti"*** walisikika wakiendesha kipindi bila kuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya uandishi na utangazaji wa habari, pale walipochambua magazeti kwa kujadili na kutoa maoni yenye kudhihaki, kukashifu na kukejeli kuhusu utaratibu wa maziko ya marehemu Askofu Dkt. Getrude Rwakatare. Vile vile katika uchambuzi huo walilinganisha na utaratibu wa mazishi ya baba Mzazi wa Waziri wa Mambo wa Ndani, Mhe. George Simbachawene (MB).

1.4 Watangazaji walishindwa kutumia weledi na maadili ya uandishi na utangazaji wa habari walipochambua magazeti kwa kuweka vionjo na maneno yenye dhihaka, kashfa na kejeli kuhusu idadi ya watu waliotakiwa kumzika Marehemu Askofu Dkt. Getrude Rwakatare pamoja na utaratibu uliowekwa juu ya maziko hayo, jambo ambalo ni ukiukwaji wa Kanuni na Maadili ya uandishi wa habari.

1.5 Watangazaji wa **WASAFI FM** walisikika wakitoa kejeli na dhihaka walipozungumza maneno yafuatayo;

**Kitenge:** ***"...nilitaka kumalizia hii ya Mtanzania Fikra Yakinifu kuhusiana na Mchungaji Rwakatare kuzikwa na Watu Kumi tuuu, watu kumi tuu, si mimi wala wewe, sisi hatupo katika hao watu kumi, aah, (hatuko kivipi jamani) aaah hii ni watu kumi tuu wewe utakuwa katika watu hao kumii?***

***Zembwela:*** ***Aaah sijatajwa, ila nilikuwa natamani sana nimzike tu***

***Kitenge:*** ***Najua najua ulitamani sana sababu ni mchungaji wetu na nini, lakini watu ni kumi tu wasiozidi kumi tuu.***

***Zembwela:*** ***Na mimi ni mmoja kati ya watu ambao ni mhudhuriaji mzuri kwenye mazishi kuliko sherehe nyingine yeyote ile.***

***Kitenge:*** ***Sasa! Aaah! Aah! kwa hili pumzikaa kwa hilii aah***

***Zembwela:*** ***Na ni mtaalamu kwenye chorus (anaanza kuimba) amerudi tena tuwaombee mamaa oooh!.*** (*Zembwela anaomboleza kwa kufanya mzaha anatoa sauti kama ya kilio kwa ajili ya msiba wa mama Rwakatare*)

***Kitenge:*** ***Aaah basi basi basii aah basi basi***

***Zembwela:*** ***(Anaendelea kuimba) ..Amerudi eeeh!***

***Kitenge:*** ***(aahh basi basi basi basi aaah basi basi unajua ndimu bwana usituamshe bwana unajua mambo haya mazito) kwa hiyo watu wasiozidi kumi tu***

***Zembwela:*** ***Ni kwa sababu ya Coron..., eeh yaa nanii eeeh maambukizi, si maambukizi***

***Kitenge:*** ***Aaah haaa haaah usiniulize bwana, watu wasiozidi kumi, maana unaweza ukaniuliza hilo halafu ukaja kwa magazeti mengine ukaniambia aaaah! mbona habari picha leo naona hapa uk 2 gazeti la majira kwamba Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene anaonekana na na mkewe, Mariana Simbachawene wakiweka picha ya baba Mzazi wa waziri huyo marehemu, Boniface Simbachawene wakati wa Ibada ya maziko katika Kijiji cha Pwaga kilichopo jimbo la Kibakwe wilayani Mpwapwa, Mkoani Dodoma, maana yake sasa unaweza ukaja huku ukaniuliza huku bwana huku mbona imekuwa vipi aaah aaah!***

***Zembwela:*** ***Huenda huko kwa marehemu mama Rwakatare wanafuata taratibu za kutokuwepo na mikusanyiko na huenda huko wamevunja taratibu, yote yanawezekana***

***Kitenge:*** ***Aaah aaah aaah hapana hapana hapana***

***Zembwela:* *Yote yanawezekana! Nimetumia neno huenda***

***Kitenge:*** ***Aaah aah aah (huenda) wewe unajua wewe mtata mtata, nakufahamu mimi ndio maana nimekuambia watu wasiozidi kumi tu! Usiniulize maswali menginee...aaah aaah***

***Zembwela:* *Lazima nikuulizee***

***Kitenge:*** ***Aaah aaaah aaah.......***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha kusoma na kuchambua magazeti kwa kutumia lugha yenye dhihaka, kashfa na kejeli kwa wafiwa kuhusu utaratibu uliowekwa wa maziko. Kituo cha **WASAFI FM** kinatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 11 (2) (a) & (g) na 30 za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018, zinazosomeka kama ifuatavyo:-

*11(2) A licensee shall not broadcast any matter which-*
- *(a) contains the use of offensive language, including profanity and blasphemy;*
- *(g) communicate a message to viewers or listeners which is likely to influence their minds without their being aware of what has occurred.*

*30.- A free-to-air content services licensee shall ensure that any commentaries that are broadcast, whether the comments are made by the licensee or by any person invited by the licensee, are presented in a manner that clearly indicates that they are based on facts which are clearly stated.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

Tarehe 23 Aprili, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **WASAFI FM**, wito wa kufika mbele ya Kamati na kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria kwa tuhuma hizo.

Tarehe 23 Aprili, 2020, Saa 10:30 alasiri, uongozi wa **WASAFI FM** ukiongozwa na Bw. Nelson Kisanga, Msimamizi wa Vipindi vya Redio **WASAFI FM** akiwa ameambatana na Bw. Hillary Daudi Mtuta (Zembwela), Mtangazaji, walifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao.

## 4.0 KUANGALIA MAUDHUI YA WASAFI FM

Kamati ya Maudhui pamoja na Uongozi wa **WASAFI FM** walipata fursa ya kuangalia maudhui yaliyotangazwa na **WASAFI FM** kupitia kipindi chao cha ***"Goodmorning Habari ya Asubuhi"*** katika kipengele cha ***"Kurasa***

***za Magazeti***" kilichorushwa tarehe 22 Aprili, 2020, saa 02:00 asubuhi ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

## 5.0 MAELEZO YA UTETEZI YA WASAFI FM

Uongozi wa **WASAFI FM**, ukiongozwa na Bw. Hillary Daudi Mtuta (Zembwela) ulitoa utetezi wao wa mdomo ambapo Bw. Mtuta aliiambia Kamati kuwa haikuwa dhamira yao kuikwaza jamii kwani sio mara yao ya kwanza kusoma habari magazateni na kisha kuitengenezea picha jongefu fupi ya kuchekesha (short comedy) kwa lengo la kufikisha ujumbe na kuelimisha jamii kuhusu jambo linalotokea kwenye jamii.

Alidai kuwa wakati wakipitia magazeti na kabla ya kwenda hewani, walijiuliza ni namna gani ya kufikisha ujumbe kwa watu wengi ambao walimzunguka marehemu Mama Rwakatare na wangependa kwenda kwenye msiba, lakini kwa sababu ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ilikuwa haiwezekani na ni lazima kuheshimu Mamlaka ambayo ilipanga ni watu kumi tu.

Aliendelea kudai kuwa dhumuni lao lilikuwa ni kuelimisha jamii lakini kukawa na ukakasi kuhusu namna walivyowasilisha maudhui yao. Hawakuwa na lengo la kutaka kuikwaza jamii au kuvunja Sheria na Kanuni.

Kwa upande wake, Bw. Nelson Kisanga alisema kuwa huwa wanapenda kufikisha ujumbe kwa jamii kwa njia ya picha jongefu fupi za kuchekesha kwa sababu wanaamini kuwa jamii inahitaji ubunifu. Aidha aliendelea kudai kuwa dhumuni na nia yao haikuwa mbaya lakini imetafsiriwa vibaya na jamii.

Alimalizia kwa kuiomba Kamati isichoke kuwaelimisha na kuwafuatilia katika kazi zao. Alikiri kuwa wamekosea katika kutoa maudhui yaliyoleta tafsiri mbaya. Aliomba radhi na kuahidi kuwa watajirekebisha ili kuwa mfano mzuri wa kuigwa katika jamii.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Baada ya kusikiliza utetezi wa **WASAFI FM,** Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **WASAFI FM** ilitangaza maudhui yenye lugha ya kukashifu, kudhihaki na kukejeli utaratibu na mipango ya mazishi ya marehemu Dkt. Getrude Rwakatare kinyume na Sheria, Kanuni, weledi, miiko na maadili ya uandishi na utangazaji wa habari;

6.2 Kamati imeona kuwa lugha iliyotumika kuwasilisha maudhui hayo ililenga kuipandikiza jamii hisia za sababu za kifo cha Dkt. Getrude Rwakatare.

6.3 Kamati imeona kuwa hoja ya kwamba maudhui ya kipindi yalikuwa ya kiubunifu na kwamba hayakuwa na dhamira mbaya bali yametafsiriwa

vibaya na jamii haina msingi wo wote kwa sababu ubunifu wao haukuzingatia wakati na unyeti wa tukio husika na hivyo wameshindwa kuzingatia weledi na maadili ya uandishi na utangazaji wa habari.

## 7.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **WASAFI FM**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **WASAFI FM** kupitia kipindi chao cha ***"Goodmorning Habari ya Asubuhi"*** imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

**Hivyo Basi**, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo kwa **WASAFI FM;**

1. Kupewa Onyo Kali na wanaamuriwa kuyaondoa maudhui hayo katika chaneli yao ya Youtube;

2. Kuomba radhi kwa wasikilizaji wa redio yao kwa siku saba (7) mfululizo kuanzia leo, kupitia kipindi chao kilichotumika kutendea kosa hili; na

3. Kulipa faini ya **Shilingi Milioni Mbili (TZS. 2,000,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **24 Aprili 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

Uamuzi huu umesainiwa na:

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**Joseph Method Mapunda**

..........................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

**Abdul Ramadhani Ngarawa**...................................

**Derek Kaitira Murusuri**......................................

**Jacob Gregory Tesha**.........................................